



UJUMBE KWA VYOMBO VYA HABARI

EMBAGO

Yaliyomo katika taarifa hii kwa vyombo vya habari na ripoti inayohusiana nayo hayapaswi kunukuliwa au kufupishwa katika machapisho, matangazo au vyombo vya habari vya kielektroniki kabla ya tarehe **16 Agosti 2023, saa 3 asubuhi London**

(11 asubuhi New York, 5 asubuhi Geneva, 6 mchana Nairobi)

UNCTAD/PRESS/MA/2023/005

Asili: Kiingereza

UNCTAD YAELEZA JINSI AFRIKA INAWEZA KUWA

KITOVU CHA UGAVI WA KIMATAIFA

Geneva, **10 Agosti 2023** – Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCTAD) litaeleza jinsi nchi za Kiafrika zinaweza kuwa washiriki wakuu katika minyororo ya ugavi duniani katika [Ripoti yake ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika 2023](#) itakayozinduliwa tarehe 16 Agosti.

Juhudi za kuimarisha minyororo ya ugavi duniani kufuatia misukosuko ya hivi majuzi zimefungua fursa kwa Afrika kuwa kivutio cha utengenezaji wa viwanda vinavyotumia teknolojia kubwa.

Wingi wake wa madini na vyuma muhimu, vipengele mwafaka katika tasnia zinazotumia teknolojia nyingi, unaweka bara hilo kama kivutio cha utengenezaji.

Minyororo ya ugavi inajumuisha mifumo na rasilimali zinazohitajika ili kuendeleza, kuzalisha na kusafirisha bidhaa na huduma kutoka kwa wasambazaji hadi kwa wateja.

Uzinduzi mkuu wa ripoti hiyo utafanyika Nairobi, na mikutano mingine ya waandishi wa habari huko Dakar na Geneva.

Kuhusu UNCTAD

UNCTAD ni shirika la biashara na maendeleo la Umoja wa Mataifa. Inasaidia nchi zinazoendelea kufikia manufaa ya uchumi wa utandawazi kwa haki na kwa ufanisi zaidi na kuziwezesha kukabiliana na vikwazo vinavyoweza kutokana na ushirikiano mkubwa wa kiuchumi.

Inatoa uchambuzi, inawezesha ujenzi wa maelewano na inatoa usaidizi wa kiufundi kusaidia nchi zinazoendelea kutumia biashara, uwekezaji, fedha na teknolojia kama njia za maendeleo jumuishi na endelevu.

Wanahabari walio na uwezo wa kufikia [chumba cha habari pepe cha UNCTAD](#) wanaweza kupakua maandishi kamili ya ripoti hiyo pamoja na taarifa kwa vyombo vya habari.

Kufikia chumba hicho pepe kunahitaji nenosiri. Ili kupata moja, tafadhali jaza [fomu ya mtandaoni](#).

Baada ya kuondolewa kwa embago, nyaraka zinazohusiana na ripoti hiyo zitapatikana kwenye tovuti kuu ya [UNCTAD](#).

UNCTAD/PRESS/MA/2022/001

Ukurasa wa 2

Kwa habari zaidi au kuomba mahojiano na wataalamu wa UNCTAD, tafadhali wasiliana na Catherine Huissoud (+41 22 917 5549, catherine.huissoud@unctad.org).

*** ** ***